

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA**

**17 MEI, 2018**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA – TAREHE 17 MEI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**261. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-  
*Hepatitis* ni ugonjwa hatari usiofahamika vizuri kwa Wananchi walio wengi:-

- (a) Je, dalili za ugonjwa huo ni nini;
- (b) Je, ugonjwa huo una chanjo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**262. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NGOMBALE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Moja ya majukumu makubwa ya Serikali ni kulinda raia na mali zao kupitia vyombo vyake vya ulinzi na Usalama ikiwemo Polisi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukirejesha Kituo cha Polisi katika Tarafa ya Kipatimu Wilayani Kilwa ambacho kilihamishwa.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**263. MHESHIMIWA AMINA NASSORO MAKILAGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Wavuvi wadogo wadogo hawana teknolojia rafiki inayowawezesha kuvua kwenye maeneo yenye samaki wengi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha maeneo ya uvuvi kwa kutumia teknolojia rafiki kuweka vifaa vya kuvulia samaki (*Fish Aggregating Devices*) ili kuongeza upatikanaji wa samaki.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**264. MHESHIMIWA WILFRED MUGANYIZI LWAKATARE (BUKOBA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kufuatia kuzama kwa Meli ya MV Bukoba, kuharibika kwa meli za MV

Victoria na MV Serengeti ambazo zilikuwa zikitoa huduma ya usafirishaji abiria na mizigo kati ya Mwanza na Bukoba kwa gharama nafuu katika Mkoa wa Kagera:-

- (a) Je, ni lini meli za MV Victoria na MV Serengeti zitamalizika kufanyiwa matengenezo yenye viwango vya uhakika ili zianze kutoa huduma;
- (b) Je, ni lini ahadi ambazo zilianza kutolewa na Serikali ya Awamu ya Tatu tangu kuzama kwa MV Bukoba za kununuliwa kwa meli mpya zitatekelezwa.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**265. MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (SONGEA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wananchi wa Kata ya Matogoro na Kata ya *Seed Farm* wanaidai Serikali fidia inayotokana na Serikali kutwaa ardhi yao katika Bonde la Mto Ruhira na mpaka sasa bado hawajalipwa fidia ili wapate ardhi mbadala:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawalipa Wananchi hao fidia stahiki;

(b) Je, Serikali ipo tayari kulipa riba inayotokana na ucheleweshaji wa kulipa fidia ya ardhi kwa Wananchi hao.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.



**DODOMA  
17 MEI, 2018**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**